BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tano – Tarehe 16 Mei, 2023
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2023/2024.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji kwa Mwaka 2023/2024.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

115. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Kumekuwa na malalamiko kuhusiana na upangaji wa mishahara mipya kwa kada mbali mbali na kwa watu mbali mbali wenye kada zinazofanana. Mfano mzuri ni kupangwa madaraja na vima vya mishahara mipya kwa walimu waliohitimu Shahada ya Sayansi katika Teknolojia ya Habari na Ualimu (BSc in IT with Education). Jambo hili linavunja moyo na kupunguza morali ya

kazi kwa baadhi ya watendaji wakiwemo walimu.

(a) Je, Shahada ya Sayansi katika Teknolojia ya Habari na Ualimu (BSc in IT with Education) ni shahada ya sayansi au ya sanaa.

(b) Je, kwa nini watumishi waliohitimu Shahada ya Sayansi katika Teknolojia ya Habari na Ualimu (BSc in IT with Education) walioajiriwa kama walimu wanatambulikana kama waajiriwa katika shahada za Sanaa wakati walioajiriwa katika kada nyengine wanatambulikana kama waajiriwa katika Shahada za Sayansi.

(c) Je, ni lini Serikali itawatambua kwa usahihi walimu waliohitimu Shahada ya Sayansi katika Teknolojia ya Habari na Ualimu (BSc in IT with Education) na kuwalipa malimbikizo yao ya tafauti za mishahara yao.

<u>Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:</u>

60. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Tabia za kuingiza magari ya ng'ombe na punda imekuwa ni moja kati ya mambo yanayotuchafulia mandhari ya miji yetu pamoja na kusababisha ajali zinazoweza kuepukika.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuiondoa tabia hii.

(b) Je, Serikali ina mikakati gani katika kulitokomeza kabisa tatizo hili.

<u>Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:</u>

63. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Wananchi na vijana mbali mbali wameamua kuitikia wito wa Serikali yao kwa kujiajiri wao binafsi kwa kufanya shughuli mbali mbali zinazowaingizia kipato ikiwa ni pamoja na waosha magari na vijana walioajiriwa katika mikahawa mbali mbali ya mama lishe. Pamoja na juhudi zao hizo, vijana hawa wanakabiliwa na manyanyaso katika shughuli zao.

Je, ni lini Wizara yako itafuatilia na kutatua changamoto zinazowakabili vijana hawa ikiwa ni pamoja na manyanyaso wanayoyapata kutoka kwa mabosi wao na watu wengine.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

25. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili, na Mifugo:

Je, ni lini Mradi wa Umwagiliaji katika Bonde la Dobi Wawi utakamilika na kuwanufaisha wananchi wengi zaidi.

**Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:**

47. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Kwa kuwa kumekuwa na mchanganyiko wa taarifa za kitakwimu kupitia Wizara tofauti zenye kufuatilia taarifa za udhalilishaji.

(a) Je, Wizara yako inashirikiana vipi na Wizara nyengine katika kukusanya taarifa kwa usahihi.

(b) Ni nani hasa anayepaswa kuwa na taarifa ya mwisho iliyo sahihi kati ya Wizara zetu zinazohusiana na maswali haya.

(c) Ni kwa kiasi gani tunauzungumzia udhalilishaji kwa sasa.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

48. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Licha ya kutopita muda mrefu tokea kufanyika kwake, Serikali iligawa boti kwa wavuvi katika maeneo mbali mbali nchini kwa dhamira ya kuinua mchango wa sekta ya uvuvi katika pato la taifa, kuongeza kipato cha wavuvi na kupunguza bei ya samaki kwa wananchi.

Je, tathmini ya awali ya Serikali inaonesha ni kwa kiasi gani zoezi hili limeleta tija kwa nchi yetu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

41. MHESHIMIWA ABDALLA ABASI WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Kwa kuwa vilabu vya mpira wa miguu vimeenea hadi vijijini na huko ndiko vipaji vingi sana vinakopatikana, kiasi ambacho kama ZFA na CHANEZA watavifuatilia na kuvitambua vipaji hivyo, wataweza kuwapata wachezaji wa timu ya Taifa walio bora zaidi.

Je, kuna jitihada gani ambazo zimechukuliwa na ZFA na CHANEZA ili kuvitambua na kukuza vipaji hivyo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

130. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika kuboresha na kuhakikisha uchumi wa Zanzibar unaimarika inavyostahiki na sekta ya utalii, Serikali iliamua kuyaimarisha maeneo ya kihistoria na kuwavutia watalii wa ndani na nje. Moja kati ya maeneo hayo ni eneo la Kwa Bikhole liliopo Bungi. Hata hivyo, mradi huo umechukua muda mrefu.

(a) Je, mradi wa kuliendeleza na kuliimarisha eneo la kihistoria la Kwa Bikhole umefikia wapi, umegharimu kiasi gani na kwa mawanda (scope) yepi ya kazi.

(b) Je, mradi huu umekwamishwa na jambo gani.

(c) Je, ni lini mradi huu utamalizika na kufunguliwa ili uweze kuingizia Serikali mapato sambamba na kuhudumia wananchi kama ilivyokusudiwa.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Kazi, uchumi na Uwekezaji kwa mwaka 2023/2024.

**Zanzibar,**
**16 Mei, 2023.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**